HABARI LEO UK4.

# Sh bil 4/- kufundisha vijana kufuga kibiashara




Na John Nditi, Morogoro

SERIKALI kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imatenga Sh bilioni nne kuwezesha vijana kupata mafunzo ya ufugaji wa kisasa katika vituo atamizi vinane kwenye mikoa ya Tanga, Mwanza na Kagera.

Vituo hivyo vinasimamiwa na Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) na Wakala ya Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo Tanzania (LITA).

Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Mifugo), Tixon Nzunda alisema hayo kwenye Chuo cha Mafunzo ya Mifugo Kampasi ya Morogoro wakati akifunga mafunzo ya wasimamizi wa vituo atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa vijana.

Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) inaeleza kuwa chama hicho kinatambua kwamba mageuzi ya kujenga uchumi wa viwanda ni lazima yaendane na mageuzi ya kuongeza tija kwenye kilimo, ufugaji na uvuvi.

Katika ukurasa wa 23 ilani hiyo inaelekeza kuwezesha vijana, wanawake na makundi mengine ya wajasiriamali kujiajiri kwa kuwapatia mafunzo na stadi za ujasiriamali na usimamizi wa shughuli za kiuchumi na kuwezeshwa kurasimisha shughuli zao ifikapo mwaka 2025.

Mpango wa maendeleo 2021/2022- 2025/2026 umepanga kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa katika uzalishaji na utafutaji wa masoko ya mazao ya mifugo,kuwezesha utafiti katika uzalishaji wa mifugo, mazao ya mifugo, uhifadhi wa mbegu na urutubishaji vinasaba, kuboresha taasisi za mafunzo ya mifugo na mitaala na kuwezesha upatikanaji wa huduma bora za ugani katika ngazi za vijiji na kata.

Nzunda alisema serikali imefungua milango kwa vijana kupitia sekta ya mifugo na kwamba vituo hivyo vitasaidia kuwabadilisha kifikra kuhusu ufugaji.

Aliwaagiza LITA na TALIRI waanze kutekeleza kazi hiyo leo Septemba 26, na kwamba fedha zilizotolewa kwa kazi hiyo zisitumike kwa ajili ya kuendeshea ofisi au kazi nyingine.

Nzunda alisema vijana wanaopata mafunzo hayo ni waliohitimu masomo ya taaluma ya mifugo katika ngazi ya astashahada, stashahada na shahada na sasa wapo mitaani hawana kazi.

Nzunda alisema vituo hivyo vitasaidia kupunguza tatizo la ajira, kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kuzingatia viwango, kuongeza kipato cha vijana na Taifa kwa ujumla.

Alisema mafunzo yataanza kwa mwaka wa fedha 2022/2023 na katika awamu ya kwanza vijana 240 wamesailiwa, ng'ombe 2,400 zitatunuliwa na kila kituo kitapewa ng'ombe 300.

Nzunda alisema kila kituo kinakuwa na washiriki au wawekezaji 30 wa kiume na wa kike na kila mmoja atapewa mifugo 10 wa kuwalea.


“Mifugo hii baada ya kuilea atakuwa wanawauza baada ya miezi mitatu na fedha zake anazifungulia akaunti na wataendelea hivyo kwa kipindi cha miezi 12 na faida watakayoipata itakuwa ni sehemu ya mtaji wao wenyewe, serikali haitachukua hata shilingi bali itabakiwa na mtaji wake” alisema.

Nzunda alisema vituo hivyo vitasaidia kuwabadilisha vijana kifikra kuhusu ufugaji, kupunguza tatizo la ajira, na kuongeza uzalishaji wa mifugo na mazao yake kwa kuzingatia viwango na kuongeza kipato cha vijana na taifa kwa ujumla.

“Vijana hawa wanakwenda kupatiwa ujuzi kuhusu maisha, ujuzi kuhusu uzalishaji wa kazi, ujuzi wa uzalishaji fedha, ujuzi wa kupata mitaji, na ujuzi wa kwenda kujenga uchumi wa nchi kupitia Sekta ya Mifugo,” alisema.

Nzunda aliwataka vijana waliochaguliwa kujiunga na vituo atamizi wajitume na wajitambue wao ni wawekezaji kwenye sekta ya mifugo.

Akizishauri taasisi za kifedha ziwasaidie vijana kuingia kwenye ujasiriamali hasa sekta ya mifugo kwa kufuga kisasa kwa kuwapatia mikopo.




Alisema jukumu la serikali ni kutoa fedha na kuwaandalia mazingira ya kuwaweka pamoja kwa kuunda vyama vidogo vya ushirika vya wafugaji ili waanze kufuga kisasa na kuweza kukopesheka.

Aliwaagiza wasimamizi wa vituo atamizi vya ufugaji mifugo kibiashara kwa vijana hao kuwa wabunifu na kuhakikisha wanasimami utekelezaji wa mwongozo uliotolewa kuhusu vituo hivyo.

Aliwataka kuwajenga vijana hao kuwa na uwezo wa kufuga kisasa kwa vitendo, kuwa na uhusiano na mawasiliano mazuri ambayo yatawasaidia katika masoko ya mifugo na mazao ya mifug.

Mtendaji Mkuu wa Wakala ya Vyuo vya LITA, Dk Pius Mwambene alisema wakala unaanzisha vituo sita katika kampasi za Kikulula (Kagera), Mabuki (Mwanza) na Buhuri (Tanga) na kila kituo kitachukua vijana 30 watakaofundishwa kwa miezi 12 kufuga kibiashara.

Mtumishi wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO), Dk Moses Olenesele aliwataka vijana waitumie fursa hiyo vizuri kwa kuwa serikali imeweka matumaini kwa vijana hao kuja kuwa wafanyabiashara wakubwa.




# Tanzania yaishukuru India

HABARI LEO UK 19.



ta

ndoa
msongo
ahusika,
ojia na
muele-

ka pia
vu ku-
ao ili ku-
ichumi
nikopo
ayotole-
..



# DED asisitiza sheria za ufugaji mijini

**Na Editha Majura, Musoma**

MKURUGENZI wa Halmashauri ya Manispaa ya Musoma mkoani Mara, Bosco Ndunguru ameagiza wananchi wazingatie sheria za ufugaji mijini, ili kunusuru mazingira hususan yanayozunguka miradi ya maendeleo.

Alitoa agizo hilo juzi baada ya kukuta mifugo kwenye majengo ya shule mpya ya Sekondari ya Kigera, akawaomba wanaoishi jirani na miradi hiyo kuilinda.

Sekondari hiyo mpya inajengwa na serikali kupitia Mpango wa Uboreshaji Elimu - Sekondari (SEQUIP), ambapo Manispaa hiyo ilipokea Sh milioni 470 kati ya Sh milioni 600 inayotakiwa kukamilisha ujenzi huo.

Gazeti hili lilishuhudia mbuzi wengi wakiwa wamefungwa kamba kwenye mazingira hayo na wengine kuzurura hovyo huku vinyesi vyao vikiwa vimetapakaa mpaka ndani ya baadhi ya majengo.

Akizungumzia changamoto hiyo kwa njia ya Simu, Ofisa Mtendaji wa Mtaa wa Kigera, Jumanne Patrick alisema elimu kwa umma inatolewa kwa njia mbalimbali kuhusu aina ya ufugaji unaotakiwa kufanyika maeneo ya mijini lakini wafugaji wanakaidi.

HABARI LEO UK 20.

# Kilwa kufuatilia pweza kielektroniki

Na Mwandishi Wetu, Kilwa

HALMASHAURI ya Wilaya ya Kilwa inaanzisha mfumo maalumu wa kufuatilia biashara ya pweza kielektroniki kuanzia wanapovuliwa, kusafirishwa hadi wanapouzwa kupitia madalali.

Kauli hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo Eston Ngilangwa wakati akizungumzia hatua zinazochukuliwa kuhakikisha kwamba wilaya hiyo inatumia vyema mpango wa serikali wa uchumi wa buluu ili kutanua soko la samaki pweza na hivyo kuboresha maisha ya wananchi.

Akizungumza na waandishi wa habari Mkurugenzi huyo alisema hatua mbalimbali zinazochukuliwa na Serikali ya Awamu ya Sita kuhusu uchumi wa buluu zimelenga kuhakikisha kwamba samaki wa Tanzania wanapata soko katika soko la kimataifa na kuwa na uvuvi endelevu.

Alisema ili kuwa na soko endelevu na hasa kwa sasa ambapo samaki aina ya pweza wanafanya vyema katika soko la dunia ni lazima nchi kuingia katika mfumo wa ufuatiliaji ili kuhakikisha usalama wa chakula.

Anasema ingawa pweza wa Kilwa wanasoko katika mataifa ya Ufaransa na Ubelgiji, pweza wake wameshindwa kupenya soko kubwa la Japan na Asia kutokana na kukosekana kwa mfumo wa ufuatiliaji wa usalama wa chakula.

Alisema katika mfumo huo wataweza kutumia misimbomilia ya utambuzi wa chakula na usalama wake kwa kuangalia historia na mahali walipovuliwa na mfumo wa uhifadhi.

Mkurugenzi huyo aliishukuru Serikali kupitia wizara ya Mifugo na uvuvi na wadau wa uchumi wa Buluu nchini ikiwamo shirika lisilo la kiserikali la hapa nchini la Aqua na kampuni kutoka Marekani California kwa kusaidia kuwezesha kuwapo kwa mfumo huo wa kielektroniki wa kufuatilia samaki pweza toka anapovuliwa hadi anapoingia sokoni kwa mlaji.

" Baada ya mfumo huu naona hali ya wavuvi inabadirikika katika kipindi cha miaka mitano ijayo, kwa kuwa na uhakika wa soko na hivyo kujiongezea kipato" alisema Ngilangwa.

Aliwataka wavuvi wa kutoka Somanga, Songosongo na Kilwa Kivinje pamoja na madalali kutambua faida kubwa inayoletwa na mfumo huo ikizingatiwa kwamba tayari pia serikali inawekeza mamilioni ya fedha kutengeneza Kilwa kuwa bandari ya Uvuvi kimataifa.

Alisema kuna kila sababu ya kuunga mkono juhudi za serikali ambayo pia imepanga kujenga mradi wa kukausha dagaa kisasa ili kutabnua soko la dagaa wa Kilwa. Dagaa wa Kilwa kwa sasa wana soko Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Halmashauri ya Wilaya ya Kilwa ina fursa nyingi za uwekezaji katika sekta ya uvuvi, ikiwa na eneo zuri kwa ajili ya ufugaji wa viumbe wa baharini kama samaki, kaa, kamba koche na mwani.

RAIA MWEMA
Jumatatu, Septemba 26, 2022

Uk 8.

# Mbwa, paka kuchanjwa Wiki ya Kichaa

Na Asha Mwakyonde, Dodoma

**SERIKALI** kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi imesema katika maadhimisho ya Wiki ya Kichaa cha Mbwa Duniani inatarajia kuchanja mbwa na paka 60,000.

Kilele cha maadhimisho hayo kitaifa kitakuwa jijini hapa keshokutwa mgeni rasmi akitarajiwa kuwa Waziri wa Mifugo, Mashimba Ndaki.

Kauli Mbiu ya maadhimisho hayo inasema: 'Kichaa cha mbwa, Afya moja, Vifo sifuri'.

Pia wananchi wametakiwa kuendelea kufuatilia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, ili kupata elimu ya ufugaji mbwa na paka, ili kujua madhara ya kung'atwa na mbwa.

Akizungumza jijini hapa juzi, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Profesa Hezron Nonga alisema katika maadhimisho hayo, watatoa chanjo bure maeneo tofauti nchini.

Mkurugenzi huyo alifafanua kuwa maadhimisho hayo pia yatafanyika kwenye kanda nane huku akizitaja baadhi ya kanda hizo kuwa ni Temeke, Arusha, Iringa, Mwanza, Tabora na Mtwara, na huduma za chanjo zitatolewa bure kwa mbwa na paka.

Alieleza kwamba maadhimisho hayo yatafanyika katika vituo vyote vya huduma za mifugo nchini, na kutakuwa na huduma ya kuchanja bure mbwa na paka, ikiwa ni pamoja na kuhamasisha wananchi kuhusu ufugaji bora wa mbwa.

"Tuna maofisa mifugo nchi nzima, kila wilaya katika halmashauri 184 wao watakuwa wanatoa chanjo hizi, hivyo karibu robo tatu ya Watanzania watafikiwa na elimu hii ya huduma za kinga, zinazoendana na tahadhari ya kichaa cha mbwa," alieleza.

Aliongeza, kuwa kichaa cha mbwa kinaua, hivyo kuwataka wananchi kuzuia kwa kuchanja mbwa na paka wao kila mwaka, ili kulinda jamii.

"Epuka kuwa katika mazingira ya kung'atwa na mbwa na endapo umengatwa, osha jeraha kwa sabuni na maji mengi yanayotiririka kwa dakika 15 na kidonda kisifungwe, kisha nenda haraka kwenye kituo cha kutolea huduma za afya," alisema.

Akitoa mwenendo wa chanjo ya kichaa cha mbwa, Profesa Nonga alisema mwaka 2020/21 walichanja mbwa dozi 986,195 na paka 5,152 na 2021/22, mbwa 1,608,344 na paka 6,833.

Mwaka wa fedha 2022/23 kuanzia Julai hadi Septemba wamechanja mbwa 323,638 na paka 28,933 kwenye halmashauri 101 ambapo katika madhimisho hayo, Wizara hiyo inatarajia kuchanja mbwa na paka 60,000.

Kichaa cha mbwa ni ugonjwa unaosababishwa na virusi vya kichaa cha mbwa na huathiri wanyama wote hususan mbwa na binadamu, na hauna tiba bali unakingwa kwa chanjo na kuzingatia ufugaji bora wa mbwa.

Pia kichaa cha mbwa huambiza kwa njia ya kung'atwa na mbwa mwenye ugonjwa huo na binadamu pia anaweza kuambukizwa kwa kugusa mate ya mbwa mwenye kichaa.

All stories from
NELLY MTEMA in Dodoma

DODOMA NEWS



# Minister touts research in livestock sector

LIVESTOCK and Fisheries Minister Mashimba Ndaki has called upon the Tanzania Livestock Research Institute (TALIRI) to advocate for research to increase productivity and value addition for livestock keepers.

He gave the call over the weekend when opening the TALIRI board, saying while the government works on new livestock policy, researchers must go for studies for increasing productivity and value addition.

"You are key stakeholders as currently government works on a new livestock policy to give us clues on the needs and demands basing on researches for more productivity and improved welfare among livestock keepers," said the Minister

"We have to know what fails the livestock industry, challenges facing the livestock keepers, market demands and status of the livestock quality for better solutions."

He said the TALIRI has to be at the forefront in formulation of the new livestock policy aimed at coming up with a way forward in developing the sector.

"Taking into account the climate change effects and the human activities, we must formulate a policy which will consider the current situation of livestock market and standards of its products so that our policy could guide us according to the qualities set," he said.

TALIRI Board Chairman, Prof Sebastian Chenyambuga assured the minister that they are prepared to improve on research to bring positive impacts to the sector.

Such research, he said, would bring solutions to setbacks in the livestock sector to make it contribute more to the national economy.

Earlier, Permanent Secretary of the Ministry, Tixon Nzunda, called upon the board members to come up with a plan on how they will mobilise financial resources for conducting research.

Moreover, he said, the board must come up with TALIRI transformation plan which will cater for the current needs and demands.

RMH to offer free



Ignorance